

A Paulo na Rumi.

❖ Waraka wa Paulo kwa Warumi.

- Paulo alipeleka sadaka hiyo Yerusalemu baada ya safari yake ya tatu ya kimishionari.
- Hii huonesha kuwa waraka wa Paulo kwa Warumi uliandikwa katika mwezi wa kwanza kwa mwaka 58 baada ya Kristo wakati akiwa Korintho.
- Paulo alisikua habari za uasi wa Wagalatia waliokuwa wamekumbatia wokovu kwa matendo, Hivyo aliwaandikia waraka mkali.
- Pia alitaka kuwaonya Warumi wajiepushe na kosa hilo.

❖ Shauku ya Paulo kuzuru Rumi.

- Kwa mujibu wa Warumi 15, Kwa nini Paulo hakuzuru Rumi wakati huo??
 - (1) Alitaka keeneza Injili maeneo ambako hakukuwa na makanisa bado (fg. 20-22).
 - (2) Alihitaji kuleta sadaka Yerusalemu kutoka Makedonia na Akaya He (fg. 15:25-28)
- Paulo alipanga kwenda Spania, kuzuru Rumi njiani akielekea huko (fg. 28).
- Alitumaini angekuwa mbaraka kwa Warumi, na aliwatarajia kumsaidia kazi yake akiwa Spania (fg. 24). Kwa namna hiyo Warumi wangewabariki wengine pia.

❖ Paulo akiwa Rumi.

- Alitiwa kizuizini alipolizuru hekalu. Alituhumiwa kuwaleta watu wa mataifa barazani atrium.
- Paulo alipelekwa kwa Kaisari alikaa huko salama kwa miaka miwili. Kisha akapelekwa Rumi kwa sababu alimuomba Kaisari.
- Hapo aliweza kuhubiri kwa uhuru kwa wayahudi na wamataifa (Matendo 28:11-31).

B Kanisa huko Rumi.

❖ Kuitwa kuwa watakatifu. Warumi 1:7.

- Salamu hizo ziliandikwa kwa waumini walioko Rumi, lakini hata kwetu zina maana. Alisema sisi tu:
 - (1) Wapenzi wa Mungu. Mungu huwapenda hususani wanaoitikia upendo wake.
 - (2) Kuitwa kuwa watakatifu. Tumetengwa na ulimwengu na kuwekwa wakfu kwa Mungu kwa sababu tulimkubali Kristo na kubatizwa.
- Mungu humpenda kila mtu na amemchagua kila mtu aokolewe. Hata hivyo, ni wale tu wanao kubali wokovu ndio watakaoupokea (Waefeso 1:4; Ebr 2:9; 2 Petro 3:9).

❖ Waumini huko Rumi. Warumi 15:14.

- Paulo aliitukuza Imani ya Warumi pamoja na mambo mengine matatu:
 - (1) Walijazwa na wema. Jinsi walivyoishi ilishuhudia upendo wa Mungu.
 - (2) Walijazwa na maarifa. Walikuwa na mizizi katiba Biblia.
 - (3) Waliweza kukanyana. Waliweza kutiana moyo na kutiwa moyo na wengine.